# Usawa Wa Kijinsia

Nimechoka! Si ndiyo kwanza tumetoka kumaliza mzunguko wa uchaguzi, na sasa tuna siku kama 14 au chini ya hizo kabla ya kupiga kura.Halafu, subiri miezi kama miwili hivi, tunaanza kusikia kuhusu mbio za kuwania urais kila sekunde. Eeee!!!!!!!!! Nawambieni, masuala haya yote ya kisiasa yaniumiza kichwa (ama pengine ni kipandauso ambacho nimepata kwa masaa machache yaliyopita).Kiwacho chote kinachoumiza kichwa changu, nataka kuzungumzia uchaguzi. Sitakuelekeza wa kumpigia kura au lolote linaloekeana na hilo! Lakini nataka kutaja ukatili mkubwa utakaotuathiri sote!

Usawa wa kijinsia!

Kuna idadi kubwa ya wanawake wanaowania Urais kutoka katika vyama vyote! Ni Baraka iliyoje kwa Marekani! Hivi, tunawatilia maanani hawa wanasiasa wa kike kama tunavyowachukulia wagombea wa kiume? Ni kweli, hilo hutegemea! Inategemea kama ana sura mbaya au la. Na inategemea ambacho mpinzani wa mgombea mrembo anasema na kufanya wakati wa kampeni.

Wanachofahamu wanasiasa ambacho sisi tusio wanasiasa bado hatujakitambua ni ukweli kuwa jamii huvutwa kiurahisi na “lugha ya mahaba.” Ikiwa na maana kuwa, kama mwanamke mzuri ni mgombea na ikiwa anaringia uzuri wake ama la, watu watamwacha endapo mpinzani wake atamshambulia kwa lugha ya mahaba. Kwa mujibu wa utafiti; kama mgombea wa kiume atamshambulia mgombea wa kike ambaye ni mzuri kwa sura,kwa lugha na machombezo ya mahaba anaweza kuushusha umaarufu wa mgombea wa kike kwa asilimia 10. Kama mgombea wa kiume atatumia lugha ya kumtusi/kumdhalilisha kijinsia mgombea wa kike, anaweza kuongeza umaarufu mgombea wa kike kwa 21%

Sasa, miaka miwili iliyopita, unakumbuka mabango, sketi, picha, na picha bandia za Sarah Palin? Je unakumbuka jinsi kurasa za mbele za magazeti zilivyoonyesha miguu yake tu? Unakumbuka picha zake bandia zilizomwonyesha akiwa katika kivazi cha ufukweni? Na kulikuwa na sketi zilizokuwa zikimwonyesha kuwa huyu malkia si chochote zaidi ya mbumbumbu. Sasa, kwa nini watu wanafanya haya na mengineyo? Kwa sababu wana taarifa!

Labda wengine wanafikiri sisi kama jamii si mambumbumbu hivi, na ya kuwa hatuwezi kuvutwa kiasi hicho. Kweli? Kwa mujibu wa matokeo ya tafiti fulani, kwa habari ya mgombea wa kike ambaye ni mwanamke mzuri wa sura ambaye mpinzani wake anamshambulia kijinsia, “Anguko lilikuwa kubwa miongoni mwa wanaume na wanawake wenye umri  chini ya 50 na zaidi ya 50, na kwa wale wenye elimu ya chuo na wasio na elimu ya chuo.” Taarifa iliendelea kusema kuwa “Lugha ya mahaba ilidhalilisha fikra za mgombea wa kike, na kuwa sababisha wapiga kura kumwona kama mtu asiye na haya, uaminifu na uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

Haya yote yanamaanisha nini? Tafiti hizi zinamaanisha kwamba Taifa letu lina safari ndefu kuhusiana na usawa wa kijinsia kila tunapofika kwenye awamu nyingine ya kupiga kura. Watu wengine wasiudharau utashi wako kwa kuwaruhusu wakushawishi kwa lugha za mahaba na matusi kuhusiana na wanawake ambao watakuwa wanagombea. Kama ilivyo kwa kila mgombea, fahamu msimamo wao juu ya hoja, na piga kura kulingana na hoja. Kwa nini kumruhusu mwanamke mrembo, na kampeni zenye lugha ya kuchafuana kijinsia ili zituchanganye tusijue anachoamini na anachotaka kutekeleza.

Wako wapi watetezi wa jinsia ya kike? Unajua, upigaji mbiu, ni bora usitufanyie ukatili kwa sababu sisi ni wanawake, “tusikie tukiunguruma.” Lifuatalo ni swali ambalo nimekuwa nikijiuliza kwa miaka kadhaa iliyopita. Hivi hawa si ndiyo wanaotakiwa kuandamana na kupiga mbiu kila inapotokea “mmoja wetu,” anafanyiwa ukatili?, Nao wanazijua tafiti hizi. Kwa nini makundi haya ya watetezi wa kijinsia yanabweteka huku yakiacha baadhi ya wanawake wakidhalilishwa, kwa sababu tu wamekuwa wazuri? Kimya- kimerudisha nyuma vita yao-kwa miaka! Kwa maana, kwa kadri mwanamke mzuri mgombea wa kiliberali anapoanza kushambuliwa ndivyo mwanamke mwingine wa mlengo mwingine alivyofanyiwa. Tunafahamu kuwa watetezi wa jinsia ya kike wanakimbilia kujitetea. Walakini, kutakuwa na mamia ya waandishi wa habari walio tayari kuwauliza swali hili; “mlikuwa wapi miaka yote iliyopita wakati mwanamke huyu mzuri alipogombea, na wakati huo huo wengine walikuwa wanamdhalilisha kwa sababu ya uzuri wake?” Nadhani watetezi hawa wa kijinsia wanasubiria vita yao kubwa inayokuja, wanatakiwa waandae sababu lukuki ili Wamarekani wazinunue?

Mbali na suala chama gani kina mgombea gani aliye mzuri, sisi kama Wakristo tunatakiwa kujua kuhusu wanawake endapo: ni mbaya wa uso, mweupe, mrefu, mfupi, mnene au mwanamke mzuri mno kuliko yeyote aliyepata kutokea, tunatakiwa kufikiria na kuwachukulia wanawake kama walio sawa na mgombea yeyote wa kiume. Na tusiruhusu mabango ya kimahaba yashawishi maamuzi yetu juu ya mtu gani wa kumpigia kura siku ya uchaguzi. Kwa mara nyingine, ni suala la hoja!

Vyovyote vile, watetezi wa kijinsia wanatakiwa kumshukuru mtu mmoja kwa namna alivyo karibu. Na mtu huyo ni Yesu. Yesu amefanya mengi kwa takribani miaka 2,000 kuhusiana na usawa wa wanawake kuliko makundi ya utetezi wa kijinsia kwa pamoja. Na ingawa harakati za utetezi zimedondoka na kuweweseka, muda muafaka, katika miaka kadhaa michache iliyopita, watetezi wanatakiwa kuishukuru injili ya Yesu Kristo kwamba bado inatawala, 1 Petro 1:22-25. Katika kitabu chake, twaona Bwana alivyofundisha na kutenda kuhusiana na usawa wa kijinsia. Na makusanyiko leo yanasikia hotuba kila baada ya hotuba kuhusu usawa wa kweli kila juma, na kamwe hawamwoni aliye kichwa cha Kanisa (Wakolosai 1:18) wakiweweseka na kuanguka kutegemeana na mwonekano wa mgombea wa kike au anatokea chama gani cha siasa. Yesu alikuja kumwokoa kila mwanamke, Yohana 3:16. Na kila mwanamke atahukumiwa naye kwa kadri ile ile, Yohana 12:44-50.

Yafuatayo ni mambo muhimu manane kuhusiana na ambacho Yesu alifundisha kuhusiana na mipaka ya kijinsia katika jamii;

1. Yesu angeongea na mwanamke, Yohana 4:7-42. Katika karne ya kwanza wanaume walikuwa hawaruhusiwi kuongea na wanawake isipokuwa kama ni ndugu. Na katika mazungumzo yake na wanawake hakuwadharau na wanawake wageni hakuwachukulia kama "mbwa." Bado Yesu alimwona mwanamke msamaria kama nafsi inayohitaji kuokolewa. Alimshtua Yule mwanamke na mitume kwa kuwa mazungumzo ya uzima wa milele!
2. Yesu angewafundisha wanawake! Kama ambavyo tayari imeonekana katika Yohana 4-5. Yesu alimfundisha mwanamke msamaria. Pia, Yesu alitenga muda ili kuwafundisha Mariamu na Martha. Na hata hivyo, siku zile wayahudi waliamini kwamba ni bora kuichoma moto torati kuliko kuwafundisha wanawake. Yesu aliwatendea wanawake kama alivyowatendea wanaume! Alifanya hivyo kwa njia ya uponyaji wake, kwa njia ya kusamehe dhambi, na ushahidi mkubwa kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya wote
3. (Luka 13:16; 7:35-8:50;Yohana 3:16; Luka 2:25-38; 4:25-38; 4:31; Matendo ya Mitume 5:1-11; 17:34; 16:13-34, n.k.).
4. Yesu aliruhusu wanawake kuwa katika kikosi chake, Luka 8:1-3.
5. Yesu alionyesha kuguswa na wajane, Luka 2:36; 4:26; 18:1; 20:47; 21:1.
6. Yesu alitumia matamshi ya aina ile ile alipokuwa anaongea na wanawake na wanaume. Kwa maana ya kwamba hakutumia matamshi yaliyoonyesha kuwanyanyapaa au kuwadharau wanawake. Luka 13:16; Luke 7:35-8:50.
7. Agano Jipya linaeleza hasa hasa katika Wagalatia 3:28, "Hapana Myahudi wa Myunani, Hapana mtumwa wala huru, Hapana mtu mume wala mtu mke; Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu." La msingi likiwa ni kwamba Mungu hajali wewe ni wa kike au wa kiume. Anataka uokolewe!

Kwa kuhitimisha-Wakati mwingine utakapokuwa kwenye chumba cha kupigia kura, hoja ndiyo zikufanye uone ni mgombea yupi anayestahili kura yako! Siyo kwa kuwa mtu ni wa kiume au wa kike, mzuri au mbaya usoni au amemalizwa na mpinzani wake, kwa maana wanaweza kuonekana katika namna fulani. Tuinuke juu ya lugha za mahaba na matusi ya nguoni, na hoja ndizo tuzipigie kura!